**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA**

***Tafadhali unapojibu taja :-***

**Kumb. Na.MDC/B.20/6/31** **16/02/2026**

# T A N G A Z O L A N A F A S I ZA K A Z I

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba anawatangazia watanzania wenye sifa za kuomba nafasi za kazi saba (7) katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

## 1.0 MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II – NAFASI 02

### 1.1. MAJUKUMU NA KAZI

i. Kuchapa barua, Taarifa na Nyaraka za kawaida na za Siri;
ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa;
iii. Kutunza Taarifa za kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi nyingine;
iv. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi;
v. Kupokea majalada na kusambaza kwa Maofisa walio katika Divisheni/Kitengo/Sehemu husika.
vi. Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
vii. Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali na
viii. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya Ofisi.

### 1.2. SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa Wahitimu wa Kidato cha Nne (Form Four) au Kidato cha Sita (Form Six) wenye Stashahada (Diploma) ya Uhazili au cheti cha NTA level 6 ya Uhazili.

Aidha, wawe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 100 kwa dakika moja na kupata mafunzo ya programu za kompyuta za ofisi kama vile: Word, Excel, Powepoint, Internet, E-mail na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

**1.3. NGAZI YA MSHAHARA**

**TGS C**

**2.0 MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II - NAFASI 02**

**2.1 MAJUKUMU NA KAZI**

i. Kuorodhesha barua zinazoingia masijala kwenye rejista (incoming correspondence register)
ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya Taasisi kwenye rejista (outgoing correspondence register
iii. Kusambaza majalada kwa watendaji (Action Officers)
iv. Kupokea majalada yanayorudi masijala toka kwa watendaji
v. Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/majalada yanayohitajika na watendaji
vi. Kurudisha majalada kwenye shubaka/kabati la majalada (rack/filling/cabinets) au mahali pengine yanapohifadhiwa
vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (file tracking)
viii. Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

**2.2. SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne cha kidato cha Nne au sita ( Form IV / VI) mwenye Stashahada au NTA Level 6 ya Utunzaji wa Kumbukumbu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali, mwenye ujuzi wa Kompyuta.

**2.3 NGAZI YA MSHAHARA**

**TGS C**

**3.0 DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 03**

**3.1 MAJUKUMU NA KAZI**

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari;
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
iv. Kusambaza nyaraka mbalimbali pale inapohitajika
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari katika daftari la safari
vi. Kufanya usafi wa gari na
vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mwajiri wake

**3.2. SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa wenye cheti cha Kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C ya uendeshaji magari ambayo wamefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali pamoja na vyeti vya mafunzo vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika. Wawe wamehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha VETA au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali

**3.3 NGAZI YA MSHAHARA**

**TGS B**

**4.0 MASHARTI YA JUMLA**

i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
ii. **Waombaji wenye ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.**
iii. Waombaji wote waambatishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
iv. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V)

yenye anwani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina yawadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

v. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma, maelezo, nakala za vyeti vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya kuzaliwa, kidato cha Nne, kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.

**- Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Diploma/Certificates.**

**- Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI**

**- Computer Certificate**

**- Vyeti vya kitaaluma (Professional certificates from respective boards)**

vi. "Testmonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo zakidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**

vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa nakuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NECTA na NACTE).

viii. Waombaji kazi wa kada ya Dereva II wenye leseni Daraja E au C wanapaswa **KUAMBATISHA** vyeti vya mafunzo ya Udereva vilivyowapatia sifa ya kupata madaraja husika.

ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo **yaliyo katika Waraka Na CAC. 45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**

xi. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.

xii. Maombi yote yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa

kuingia sehemu iliyoandikwa **'Recruitment Portal').**

xiii. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **01 Machi, 2026**

xiv. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

**MUHIMU**: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa;

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba,**
**S.L.P 263,**
**IFAKARA.**

Tangazo hili limetolewa na,

**MKURUGENZI MTENDAJI (W),**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA**